REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 19st October, 2022.

The House met at the Assembly Chambers at 9.00 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

PAPERS LAID

ASSEMBLY CALENDAR

Hon. John Gichuki: Hon. Speaker, I beg to lay a paper on the calendar (Regular Sessions) of the First Session of the 3rd County Assembly of Laikipia (September to December, 2022).

(Hon. John Gichuki laid the Paper on the table)

NOTICES OF MOTION

ASSEMBLY CALENDAR

Hon. John Gichuki: Hon. Speaker, I beg to move the following motion,

THAT, pursuant to the provisions of Standing Order No. 29 (1) This House approves its calendar (Regular Sessions) for the First Session of the 3rd County Assembly of Laikipia (September to December, 2022).

MOTION

EXPOSITION OF PUBLIC POLICY IN GOVERNOR'S ADDRESS

Hon. Speaker: Hon. Members, as you know, this is our last day to deliberate and discuss on H.E the Governor's Address to the House. I therefore open the floor and invite the Members, I will prioritize with the Members who had not had a chance to give their maiden speeches to do so now and discussion on the same on Governor Address.

Hon. Catherine Nyokabi: Thank you, Hon. Speaker for giving me this chance, first is to thank the God almighty for bringing me back to this House. In the last regime, I was a Specially Elected to this House representing the Gender Top-up. Right now, I am an elected Member of County Assembly representing the people of Ngobit Ward.

I would like to take this golden chance to thank the people of Ngobit, for having faith in me and electing me back to this House being the first woman to get this position in Ngobit Ward. I would also like to take this opportunity to also congratulate you for being elected as the Speaker of this Honorable House.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

I would also like to congratulate my colleagues for getting this chance to serve Laikipians and also those one who got positions in leadership. Allow me to go straight to the speech that was given by H.E the Governor, on the official day of the opening of this Honorable House.

First is to congratulate H.E the Governor, for coming up with a noble idea that will cure a disease that has been suffered a lot in this County in the health sector. From today henceforth, there will be no problem in our County for our people to be going to neighboring Counties to seek medical services. We will be getting it in a quality manner in our County.

Mr. Speaker, I would like to quote something in his speech. The Governor stated that he will ensure that the revenue from the health facility will be for exclusive use at the respective facility through the establishment of Laikipia Health Services Facility Improvement Fund. In health sector, I would like to quote in regards to health sector personnel, plans are underway to transition competent health workers who are currently engaged on contract to permanent and pensionable status.

That means there will efficient and effective services in our hospitals but any time, our Laikipians will be going to hospitals. They will be getting services which we want and they will be quality services. To add on H.E the Governor's Speech, I would like to remind him that there were promises that he was giving our people during the campaign time. Like in my ward, we were promising them that we are going to dwell on the road network.

The roads in my ward are pathetic and impassable. We also promised them that we are going to introduce feeding programme in ECDEs. We also promised that we are going to increase the bursary fund. I congratulate him because he gave a proposal in his speech that he is going to increase the allocation in the budget for the Financial Year 2022/2023.

Fourthly, we promised our people that we are going to increase water storage. I would also like to say that I am a woman elected in this Honourable House and I will be in the forefront to support businesses that will empower our youth and women. Lastly Mr. Speaker, I whole-heartedly support the speech of H.E the Governor. I am ready to work together for the betterment of Laikipians. Thank you, Mr. Speaker.

Speaker: Thank you, Honourable Member. It was indeed a good speech. The floor is still open for Members to contribute. I am still giving a chance. So far we have 15 others who have contributed to the speech. I call upon those who have not done so that this is your opportunity to do so. If those who have contributed would like to add more clarity to the previous maiden speeches, you are welcome to do so.

Hon. Antony Theuri: Thank you, Mr. Speaker. It is a good morning and I would like to emphasize on the Governor's Speech on bursary allocation. It is true in the previous House, they only allocated Kshs.25 million which is less compared to other years. I would like to urge this House that we are going to try and come up with a different idea when it comes to bursary allocation. As I had said before, it has become a huge task for bursary allocation.

It has become purely a women's affair when it comes to the bursary, and it has become a tedious duty. The bureaucracy of getting the bursary is a workforce by itself. I would like, if possible, we sit down with these Members and try to integrate or come up with a formula. To me I would like maybe we have a one-stop office, where a parent or the beneficiary who would like to get the bursary, just walk into an office.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The same way you go to an M-PESA or a bank office. For example, you fill in your form and that deal is done. Mostly, I would like it to be more digital. In that way, we are going to see a lot of loopholes. As I had said before, that the bursary itself has become a loophole of corruption. We are using it as a campaign tool. To us it is a positive one because I would like to be more associated that Honourable so and so, during his tenure he gave us a lot of bursaries.

I would like to urge the Members, so that we can come up with maybe a loan, we pass it here that we are going to make it to each and every Ward. It is not even fair where you go to a place like Mukogodo West, Mukogodo East, and Sosian, or rather Laikipia North at large. They have been disadvantaged for a long time. I think it is the high time that when we are going to give out these bursaries we consider some things.

In my area and Hon. Kagondu can attest to this, some Wards like Thingithu, Umande and Nanyuki have a lot of people. When you are going to give out these bursaries, the Kshs.100 million, we cannot give it out equitably. If you divide it by three, it will be Kshs.25 million. At the end of the day, the people from Laikipia North will have an advantage over us. We need to come up with an idea so that at the end of the day, everyone will be accommodated. Thank you, Mr. Speaker, Sir.

Speaker: Thank you. I have few Members who have not yet given out the speeches. I would like to invite those who are ready among those who did not get a chance. Good, welcome Hon. Member.

Hon. Mary Gathoni: Thank you, Mr. Speaker. I would like to thank God, for giving me this opportunity to serve the people. I would also like to congratulate you for not forgetting to congratulate all the Members who have been elected and nominated. How I wish you will fulfil the manifesto.

I would like to briefly to the Governor's speech on health. It was a plus for him to reinstate our doctors. I would also like to give an input on the issue of their internal audit. I believe we still have a problem that needs to be handled. We are still being referred to private hospitals whereby I would suggest that we have a doctors' Plaza inside our hospital where the doctors will be literally available when there are emergencies and other services.

We are being also referred to the laboratory which is private. How I wish they will do something regarding our laboratory inside our referral hospital. On the issue of water and sanitation, I would prefer if somebody will come up with an idea of a larger catchment of water because buying tanks is not enough.

We still need to have a tangible solution, like creating more dams in our areas. For food security, I would not say that I do not advocate for the feeding program or donation of food. We need to encourage our farmers to plant drought-resistant foods like yams and cassava. This has been working for West African countries like when you go to Cameroon and Nigeria, they survive with this cassava and whatever.

When you talk about youth and empowerment, it breaks my heart to see how our youth are idle outside and nothing is being done. Most of them have dropped out of school and they are doing drugs. I do not know who will come up with a solution whereby we will stop, because cocaine is being sold just like any other groundnut outside there. It is killing our youths. Our

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mothers, fathers and sisters are crying outside there. The issue of bursaries; how I wish that it will be a fair thing when it comes to bursary allocation. Thank you, Mr. Speaker. That's all I had.

Hon. Catherine Umija: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity to just speak a little on the Governor's speech. First of all, I want to thank the Lord for this wonderful day and also the opportunity that he has given me to be able to serve the people of Laikipia.

I am looking at the Governor's speech and his six pillars on health, sanitation, youth employment, trade, and food security. I think let us be honest, if we are not able to feed our people, all these other things become secondary. We know that we have the primary needs of people that are food, health and shelter. If people are not healthy, they are not having food, not necessarily food but good food. I will just say it in Kiswahili. It is not about "*Bora chakula lakini chakula Bora"*. So we need to give our people good and healthy food.

How do we secure food security? First of all, we need to revamp our agriculture. Go back to the basics that we all know about. If we allow ourselves to invest more in agriculture, we will allow ourselves to empower the youth to take up agriculture. Leave alone Information Technology, agriculture is going to be the most profitable venture in the world.

Remember that due to climate change; most of the arable lands in the world are not able to produce enough food. So, we only remain with Africa, which has most of its land arable and we need to take up this venture seriously. This is a place where we can have youth employment if we are able to convince our youth to be able to take up agriculture in a more advanced way with the use of technology.

This is a place where we will not talk about youth not having employment, but now they will take up agriculture as part of their solutions to their problems. They will be able to be active, they will not be involved in drugs. I hope our Governor will look at it carefully as we look at the root causes of our problems.

Let us look at the root causes. The low-lying fruits, which is agriculture. This is what we have. So, if we put all our ventures on agriculture and water which goes together, then we will be able to secure food problems within Laikipia County.

Secondly, talking about health, I want to thank the Governor for taking up this issue. I remember during the last regime we had problems. I stay here in Laikipia and our nearest health service is Nanyuki Teaching and Referral Hospital. Actually, we no longer call it Nanyuki Teaching and Referral hospital. It is now called Laikipia Health Center.

You can imagine having dropped down from a referral hospital to a health centre and you are not even getting the basic service of even having Panadol, a painkiller in the hospital. It is very pathetic. It meant that people had to go to private hospitals to get their services. I thank the Governor because he has taken up the issue. He is revamping the health services within Laikipia County. This is going to be beneficial to the people of Laikipia. I would really commend the Governor on that.

Just as the other Honourable Members stated that as much as we are giving out health services, we also need to look at the budget. We look at what we can afford and also look at what we can be able to give to our people. I think once we look at the budget and look at whether it is feasible for us to put a lot of money into health services and then we will do that. Let us not forget

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

about the other structures that also need the money as well. I hope the Governor will do a balancing act on all the sectors so that we are able to balance each and every sector. Thank you, Mr. Speaker.

Speaker: Asante Mheshimiwa, Kwa mazungumzo hayo mazuri. Tungali na nafasi kwa wale ambao hawakuweza kupata nafasi za mazungumzo lakini nachukua nafasi hii kukaribisha Mheshimiwa George Karuiru.

Hon George Karuiru: Thank you, Mr. Speaker. I appreciate that now; your pronunciation is becoming better of the name Karuiru. I would like to take this opportunity to thank God for giving me this chance and as well add on the Governor's speech. Mr. Speaker, as most of the Honourable Members have said here for the last one week, I have had a hectic life. As I addressed that in the Governor's speech, there was no matters particularly touching on security.

As we all know, security is actually not devolved. There is that level of intervention or collaboration of the County and the National Government. Mr. Speaker, in the bottom-up economy the last time the Deputy President called the County Commissioners and Commanders in Nairobi. He addressed this issue through the Governors, that if they won't work together and he even assured them that they will not go anywhere. They are there to remain as long as they work with the County Governors.

Mr. Speaker, as I speak now I have received a text here that in one of my Sub-Locations named Wangwachi, there are thousands of cattle and some of my people have been forced to remove their maize plantations even before they are good for harvest. This should be addressed because as far as we might feel for our herders for lack of grass from Baringo, Isiolo and Samburu, as we are addressing matters of human hunger, even the livestock hunger should be addressed.

As we sit in this Hon. House, I appreciate that there is public participation pertaining the CIDP and I am expecting that Members have mobilized. I am proud of Hon. Members for Thingithu, the Majority Whip because he addressed this during our meeting with holders of public participation. He said that we not only need promises but address that our budgets are up to a particular level so that we do not give our people a lot of expectations that might not yield.

I believe that through the bottom-up module and as diverse as you are Mr. Speaker, and having worked with inter-governmental relations, we are going to guide that all the resources that the National Government have. There can be dams constructed from Amaya and other places. I know this issue because it is actually a signal because wherever we are harvesting in Olmoran Ward, the first signal for crisis is like what is beginning now.

Mr. Speaker, with your capacity through the Governor to the County Commissioner, there can be issues to be addressed that will deter those people that are coming to graze in those plantations.

Mr. Speaker, the other one which was not captured in the Governor's speech are the already the existing projects and mostly the affecting ones. Hon. Umija has spoken about the basic needs which we need to have. As I speak now, at least three boreholes from my area have broken down and you can see how the rains are not sufficient currently. One of my areas namely Kaharati, Mlima Meza and Olmoran Town, I believe all those Members having smart phones have seen it trending that they cannot access clean water currently because one of the fuses of those boreholes which we put are not in place.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

I would want with the capacity of the Governor to urge the treasury because for this, we cannot blame either of the sites. I have seen in papers that there has been pre-qualification of contractors, I think that it is just from the acting Chief Officers before we ascertain them to go and make sure that those breakdowns of water are looked at.

Mr. Speaker, I appreciate that the health facilities have been checked and rechecked again but at the same time there are still complaints from the medical facilities. As we budget because I know that we will get the supplementary budget, I appreciate that yesterday there was the nomination of the CECMs to be. I am hoping that you will fast-track this. I know that the House of laws can reduce or even add the days of vetting so that the soonest we have sitting CECM's and Chief Officers, we will immediately go ahead. As this issue is holding my back, I know that part of it touching on matters of water and if improved, our people will not suffer again. Thank you for giving me the second chance to speak on Governor's speech.

Speaker: Thank you, Hon. Karuiru for a good speech. It is a matter of concern that you have touched on security. We will have to give this matter precedence later so that proper measures are taken with all government agencies concerned. I want to continue asking Members to contribute. Hon. Irene Wachuka has just entered the House, welcome. Any other Member who would be willing to continue with the debate, you are welcome.

Hon. Samuel Mugambi: Thank you, Mr. Speaker. My name is Mugambi Gatati and thank you for giving me another chance to contribute. I am standing here to just add on what I echoed last week. According to the Governor's speech, there is a point which he made on youth and employment. In this Assembly, most of the elected Members and the nominated are youthful. Most of the leaders in this world just talk about youth and employment but it is easier said than done. Everywhere you go everybody is talking about the youth forming 75% of the population in this country.

Yesterday as I was following some media airing, I got that in the National Assembly they had a group of young parliamentarians meeting at Karen, the official residence of the Deputy President and they discussed very many important issues about the youth. Since I am a youth from Laikipia, I want to quote a Jamaican singer by the name Richey Spice when he was talking about wearing Gideon boots and a khaki suit in a world of Babylon so that he may stand for truth.

As Mugambi Gatati, I will stand with the youth of Laikipia because we need change and if you want change you must start with the change. I would urge by your leadership Mr. Speaker, Sir, to help us even form a youth group comprising of those MCA's who are youthful in this Assembly so that when we have agendas that are affecting the youth, we can come together as a small House and stand for the youth of Laikipia. Even this one as we start it here, I know that it will cut across even to the Executive side.

There is one time when I was standing in some developed country and this matter of youth empowerment and employment is something very important; it was even echoed in their constitution but in our case, it is just in our mouth. Therefore, I would ask the youthful guys who are sitting here with me, the Hon. Members and maybe by your guidance, Mr. Speaker, you can guide us on how to form it. I am ready and I believe that even my youthful MCA's will back me. Thank you.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Speaker: Hon. Samuel Mugambi, thank you very much for the speech. I want to give the floor to Hon. Benson.

Hon. Benson Kuria: Asante, Bwana Spika kwa sababu ya hii nafasi ambayo umeweza kunikabidhi. Ningependa kutoa shukurani zangu kwa Maulana na Wabunge wenzangu walio hapa, walioteuliwa na chama na pia wale walioweza kujikakati na kufaulu kwa sababu ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Bwana Spika, nikiweza kuingia katika hotuba ya Gavana, kuna jambo ningependa kuguzia. Niseme ya kwamba katika kitabu cha Samueli wa kwanza kuna wakati Samueli alielezewa aende katika boma ya Jesse ili aweze kuteua mfalme. Mahali pale palikuwa na watu wakubwa na wanene ambao mawazo yao na fikira zao walijihisi kwamba watapata yale mafuta. Bila shaka Biblia husema ya kwamba Samueli aliposubiri, wote walikosa na dakika ya mwisho kukatokea kijana maskini, hafifu ambaye hana lake na mafuta ikaanza kumwagika kutoka kwa pembe. Yule kijana anaitwa Daudi.

Kwa hivyo nasema ya kwamba hili Bunge la tatu tangu tupate ugatuzi, wewe ndiye Daudi mahali umetoka kwa sababu Mwenyezi Mungu alikuona wewe. Kulikuwa na mashujaa wengi wenye pesa na uwezo lakini Mwenyezi Mungu akaona ya kwamba wewe ndiwe utakayekuwa mwakilishi wa hili Bunge la tatu ili uweze kutetea watu wako. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu ndiye amefanya niwe mahali nilipo na pia wewe.

Bwana Spika, najua hata wewe ulikuwa katika ile vita na ninajua ya kwamba pale kulikuwa na vigogo wakubwa ambao mngetishana nao lakini pembe la mafuta liliweza kukuangukia ili uwe kinara wa hili Bunge. Kwa hivyo, wewe ndiye Daudi ambaye Mwenyezi Mungu aliweza kumwagilia mafuta.

Nikiguzia hotuba ya Gavana, ningependa kusema ya kwamba ukiangalia katika eneo la kwetu mahali mimi ni mzaliwa, Gavana aliguzia agenda ya maji kwa umakini sana. Alisema ya kwamba katika kila kilomita tatu kila mahali kutakuwa na maji na naomba Mwenyezi Mungu liwezekane. Lakini ningetaka kusema ya kwamba yale maeneo nimetoka na nayajua kwa majina.

Kwa mfano ukienda Ndonyoluo, ili uweze kupata maji safi unatembea karibu kilomita kumi ili uweze kufika Lonyek na labda mama ni mjamzito. Kwa hivyo wakati tunapanga ni vizuri tufikirie wale watu kwa sababu kutoka Lonyek kuenda Ndonyoluo ni kilomita kumi na tano. Kutoka Ndonyoluo kuelekea Tegeme ni zaidi ya kilomita ishirini au Lakwam. Hizo eneo zote hakuna mahali kuna bwawa la maji.

Niunge mkono Mheshimiwa George Karuiru Wairimu ya kwamba mahali pale Olmoran ambapo ni mji wangu, watu pale ni wafanyibiashara. Sasa hivi wako zaidi ya miezi miwili bila maji. Naomba tu mweka hazina ambaye anayeshikilia afanye jambo kwa sababu lile jambo ni janga ambalo limekumba mahali pale.

Unapata yule mkaaji wa hilo eneo la Olmoran inabidi aamke saa tisa ya usiku ili aende kuteka maji na sana sana hataweza kufungua kazi yake kwa sababu utapata mahali wanapochota maji wakiwa zaidi ya elfu mbili. Kwa hivyo hilo ni janga ambalo liko mahali pale na limeumiza wengi. Bwana Spika, kama kuna uwezekano, hao watu wameteseka karibu ya miezi miwili na hiyo ndiyo eneo ambalo tunategemea.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Nikitembea mahali pale niko na uchungu kuona kina mama wakongwe wakikaa chini kusubiri maji zaidi ya masaa kumi na kisha kurudi nyumbani bila maji. Ni jambo la huzuni kuona ya kwamba katika serikali ya *bottom up* kuna wale watu wa chini walioamka mapema kuchagua viongozi mahali pale wakiwa na shida tupu. Ukienda kwa hoteli na labda mwenyewe hakuwa amechota maji hauwezi ukapata chai. Hauwezi ukapewa na mtu maji katika boma yake kwa sababu atakutuma kwa duka uende ukajinunulie maji kwa sababu hauwezi ukapewa.

Kwa hivyo Bwana Spika, kama kuna uwezekano, lile ni jambo dharura na linafaa kushughulikiwa ili tone ya kwamba maisha ya wakaaji wa eneo la Olmoran yamebadilika. Asante kwa hiyo nafasi ambayo nimepata.

Speaker: Thank you, Hon. Benson Kuria. Now I want to give the floor to Hon. Salim Edung.

Hon. Salim Edung: Asante Sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi kwa mara ya pili kuweza kutoa yale mambo ambayo tuliongea hapa kuhusu hotuba ya Gavana. Kabla sijaongea hayo, nashukuru watu wa Wadi ya Segera walionipatia kura ili niweze kufika katika hili Bunge. Kulikuwa na watu wengi ambao walikuwa wanagombea viti lakini kwa mapanzi ya Mwenyezi Mungu nikafika mahali hapa na pia ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu imefanya tuwe mahali hapa.

Nitaongea tu kwa kipenge cha tatu kulichokuwa katika hotuba ya Gavana kuhusu matibabu ya hospitali. Huku kwetu Wadi ya Segera, unapata hospitali moja imejengwa kwa umbali wa kilomita ishirini au kumi na tano ilhali sisi tunasema ya kwamba ni vizuri wananchi wa Kenya wapate matibabu mahali ambapo mtu hawezi tembea takribani kilomita kumi na tano au ishirini.

Katika hotuba ya Gavana nimeona ya kwamba iliangalia sana kuhusu afya na tunaomba ya kwamba inapojengwa mahospitali katika wadi zetu, inafaa iangaliwe hakujainuka sana. Kuna mahali pengine ambako unaenda kilomita mbili unapata hospitali, unaenda kilomita mbili unapata shule au kilomita moja na kupata maji lakini sisi ambao tuko eneo la Laikipia Kaskazini, sana tumeadhirika kwa njia nyingi. Ninaomba hii serikali kupitia hili Bunge la tatu, ni vizuri pia sisi tuangalie ni watu wapi ambao wanaumia.

Hasa eneo la Lekiji hivi karibuni kulijengwa hospitali lakini madawa hakuna au anapata daktari ni mmoja. Unapoenda pumziko, lile hospitali linafungwa. Sisi tunasema ya kwamba tunahitaji matibabu yawe karibu na wananchi. Mimi ningeomba katika hiyo hotuba ya Gavana, tuangalie katika Wadi ya Segera ili mambo ya hospitali iwe karibu na wananchi.

Katika kipenge cha pili kuna mambo ya *bursary*. Katika eneo zetu, unakuta hasa wakati huu walimu wakuu katika shule wanafukuza wanafunzi kwa sababu wamekosa karo ya kulipa pale. Unakuta ya kwamba mwanafunzi wa kidato cha nne anakaa nyumbani na bado anangojea mtihani wa kitaifa.

Ukijaribu kulinganisha pamoja na wale ambao wako shuleni sasa hivi, unapata hata kwa kufanya mtihani, hatafuzu kama wanafunzi wengine na hii ni njia ya kukosa karo ya shule. Mimi ningeomba katika hili Bunge ya kwamba tunapopatiana hizo pesa milioni mia moja, tungependa sana hao wanafunzi wapate masomo bora kama wale wengine.

Kwa upande wa barabara, barabara zetu hasa kwa ile wadi ambayo mimi nimetoka hazina *murram*. Ikifikia wakati wa mvua hata wanafunzi kupitia kwa hizo barabara kuelekea kwa shule, mto mingi huanza kufurika na maji kuwa mengi. Ile ng'ambo nyingine unapata walimu au

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wanafunzi huwa hawaendi shule na masomo haiwezi kuendelea. Ningependa katika Wadi ya Segera kwa sababu hao ndio wale watu walionileta katika hili Bunge, waangaliwe upande wa barabara.

Katika hotuba ya Gavana, katika hizo vipenge sita katika hiyo daftari, niliona ya kwamba Gavana aliangalia umuhimu wa hizo vitu ya kwamba zitasaidia Mwanalaikipia. Kwa hayo mimi ninashukuru na nikomee hapo na Mungu awabariki.

Speaker: Asante Sana, Mheshimiwa Salim kwa hotuba yako nzuri na tunashukuru kwa muda ambao umechukua. Ningependa kutoa nafasi moja ama mbili kwa yeyote yule ambaye angali yuko na jambo la kuchangia katika mazungumzo ya Mheshimiwa Gavana.

Hon. Irene Wachuka: Asante Sana, Bwana Spika. Asubuhi ya leo nataka kwanza kushukuru Waheshimiwa ambao wako katika hili Bunge letu la tatu, waliochaguliwa na pia wakuteuliwa kwa sababu sisi wote ni kitu moja. Nataka pia kushukuru Mwenyezi Mungu ambaye alitupatia nguvu ya kukuchagua kama Spika wetu wa Bunge la tatu na ninajua ya kwamba tutafanyia Wanalaikipia kazi. Ninafurahia kujua ya kwamba Laikipia ni la kabila zote na kwa hayo Nashukuru Mwenyezi Mungu.

Ningetaka kuchukua hii nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Gavana ambaye ndiye baba wa hii Kaunti ya Laikipia. La kwanza ni mambo ya pesa ya ufadhili kwa sababu imesumbua watu wengi sana. Kila mtu anaona vile nchi yetu ilivyo. Nchi haina pesa, ukame umeingia hadi mifugo na watu wanakufa njaa. Kwa hivyo wakati alisema ya kwamba *bursary* itaongezwa kutoka milioni hamsini hadi mia moja, niliona ya kwamba wale wazazi ambao hawana nguvu watapata kusaidika.

Sisi kama Wabunge ambao wamepewa hilo jukumu, wakati ambapo tunaenda kugawa hizo pesa, tuweze kuangalia wale watu ambao wako chini sana kwa sababu watu ni tofauti. Kuna watu ambao husema ya kwamba hawana pesa lakini ukiingia kwa boma lake kuna kitu ambacho anaweza akashika kama mbuzi au ng'ombe na auze na kusomesha mtoto. Mambo ya *bursary* ni jambo muhimu sana.

Lingine ni mambo ya maji. Maji ni ya umuhimu sana kwa sababu maji ni uhai. Hata kabla Gavana aingie akiomba kura, tulipokuwa tukizunguka naye, kazi yake muhimu ilikuwa mambo ya maji na afya na hayo ndiyo alikuwa anatajia wananchi. Najua sasa hivi haangalii Kaunti pekee lakini anatoka hadi nchi ya Kaunti akiangalia watu ambao wanaweza kumsaidia ili watu wake wapate maji.

Jambo lingine ni kuhusu Igwamiti. Kwanza nataka kusema ya kwamba sina neno kuhusu Igwamiti. Kama kuna mtu alisaidiwa na watu wa Igwamiti ni huyu ambaye aliyesimama mbele yenu, Mheshimiwa Wachuka aka Mama yao na haikuwa kazi rahisi. Wanaume wanane dhidi ya mwanamke mmoja na wakanirudisha wakati wa uteuzi. Wakati wa uchaguzi wakawa wanaume kumi na saba dhidi ya mwanamke mmoja na hakuna hata mwanaume mmoja mbaye aliyetoboa. Hayo ni mambo ya Mwenyezi Mungu kwa sababu sio nguvu yangu au kufanya siasa kuliko wengine.

Ningetaka kusema ya kwamba Wadi ya Igwamiti ndiyo ya pili katika nchi ya Kenya iliyo na watu wengi sana kwa sababu wapiga kura ni 43,194 sasa hivi. Nilifanya siasa ya mbunge na ninaomba Mwenyezi Mungu hiyo wadi igawanywe kuwa wadi nne na kuwe na eneo Bunge la Nyahururu. Juzi kabla Gavana Ndiritu Muriithi hajatoka katika hizi maofisi, nilikutana na Chebukati pale nje wakiwa na yeye na nikaongea mambo ya Igwamiti. Igwamiti ilikuwa katika

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Manispaa ya Nyahururu na ilikuwa na wadi sita na kuongezwa zingine mbili zikafika wadi nane na huo wakati nilikuwa Naibu wa Diwani katika Manispaa ya Nyahururu.

Nashukuru Gavana wakati alikuwa anasoma hotuba yake nilisikia akitaja Manispaa ya Nyahururu itakuwa na bodi ambayo inaitwa *Board of Management of Nyahururu Municipal* na Nanyuki. Wakati ilikuwa Baraza kulikuwa na Manispaa mbili ya Nanyuki na Nyahururu. Wakati Gavana aliyekuwepo alikuja hapa na kuitoa na kuipeleka Wadi ya Rumuruti. Ilisemekana hiyo bodi itaenda huko. Tuliridhika na sasa Mungu ametuletea Musa ambaye ni Joshua Irungu ambaye alisema Nanyuki na Nyahururu itakuwa na Bodi ya Usimamizi.

Pili, kuna jambo ambalo halikutajwa la muhimu sana katika Kaunti ya Laikipia ambalo ni vyuo vikuu. Laikipia nzima iko na chuo kikuu kimoja cha Laikipia. Kwa sasa mahali tumeelekea naomba Waheshimiwa wenzangu watusaidie. Gavana aliyekuwepo alichukua wafanyikazi 75 na kuwapeleka Chuo Kikuu cha Kimathi.

Basi zilikuwa zinatoka Chuo Kikuu cha Kimathi, zinachukua wafanyikazi na kuwapeleka huko mafunzo kwa miaka miwili. Pesa yote ya Laikipia ilienda Kaunti ya Nyeri. Hiyo ni haki kweli? Naomba Waheshimiwa wajue hiyo ni dhahabu tuko nayo. Hata kama iko Magharibi mwa Laikipia, hicho chuo si cha watu wa Igwamiti bali ni cha watu wa Laikipia. Hiyo ni kitu muhimu sana na mahali tunaelekea, juzi nimekuwa na Gavana ambaye nilimtafuta hadi nyumbani na ningetaka twende huko.

Hata kama kuna kazi ya kufagia huko, Makamu mkuu wa Chuo hawezi kupatia watu jirani kazi ila zinapatiwa watu wa kutoka nje. Rais wa zamani Kibaki alipeana hiyo shule na watu wa Igwamiti waliinuka sana. Kama uko na shamba, unakata ploti na kujenga hosteli. Kwa hivyo hii shule inasaidia watu wa Laikipia nzima. Naomba Naibu wa Spika hata kama ametoka akae akisikiza. Kuna maneno ambayo inaendelea na ningetaka kuwe na Chuo cha Laikipia katika Nanyuki ili watu ambao wako hapa wasaidike.

Hata kama ni wafanyikazi hapa, watatoka kazini jioni waende wakasome. Hiyo ni muhimu sana na naomba Waheshimiwa wakati tutakuwa na mkutano na Gavana, wangoje wakati nitaongea kuhusu Chuo Kikuu cha Laikipia ili muniunge mkono. Hicho chuo kikuu kikikuja hapa wafanyikazi wa hapa watendelea na masomo yao. Mimi niko mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Laikipia. Vijana wananichekelea lakini mimi naendelea kusoma.

Nilishtuka sana kuona Gavana aliyekuwepo akichukua mali yetu yote lakini mali ambayo inapelekwa Kaunti ya Nyeri ni mingi sana. Basi zilikuwa zinasimama hapa na kuchukua wafanyikazi kwa miaka mbili na hiyo ni mali yetu. Ndio maana unaona hii Kaunti imesimama. Naomba wakati tutakuwa na mkutano na Gavana, Waheshimiwa wote 21 wakati nitatoa huo mjadala muniunge mkono.

Kuna Shule ya Upili ya Ndururumo ambayo Noordin Haji alisomea. Pia alisomea Shule ya Msingi ya Elite. Upande ule mwingine wa Chuo Kikuu cha Ndururumo kuna sehemu ya kutupia takataka kubwa ambayo inaathiri walimu na watoto wa Ndururumo. Afya ni kitu muhimu. Niko na mambo mengi sana ya Igwamiti kwa sababu sikupelekwa Igwamiti lakini nimezaliwa huko, nimeolewa huko na nimesomea huko. Kwa hivyo mimi ni mwanzilishi wa Igwamiti na najua ni nini kinakula kile kingine.

Waheshimiwa ambao wako karibu kama vile Mheshimiwa Gatati na Mheshimiwa John, wakati mnapita huko muniulize mahali mtanishikilia. Waheshimiwa tushikane kwa sababu huo

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mji ni wetu. Haikuwa kazi rahisi kupigana na Matiang'i kwa sababu kutoka 1990, Nyahururu ingekatalia Nyandarua.

Ingechukua masaa manne nipige nduru lakini Rais Uhuru akaambia Matiang'i aangalie ni kwa sababu gani mama yao anapiga duru. Hiyo siku nilikuwa nimeamua kufa ama kufungwa lakini Nyahururu ni lazima ingerudi Laikipia. Serikali ikitaka kufanya kazi, inaweza kufanya. Matiang'i alikuwa hapa kwa sababu ya usalama wa Wadi ya Ol Moran. Nilimuuliza kama hapa ni Ol Moran na ilifaa aende Ol Moran mahali ambapo kuna vita.

Aliuliza ni nani huyu, nikamwambia ni mimi. Nilipiga nduru na kuanza kulia. Akaniuliza mambo mawili ya kusaidiwa. Nilimwambia jambo la kwanza nataka kusikia Nyahururu imetoka Nyandarua. Ndege tatu zilikuja kwa masaa nne na Nyahururu ikarudi Laikipia. Ni kazi nimepigana na uongozi si kitu cha kuchukulia kwa urahisi.

Ukiona mtu anaenda kwa uwanja kutafuta kiti, usimchezee Bwana Spika. Najua unajua kwa sababu tulikuwa na wewe kwa serikali ya kwanza ya Gavana Joshua Irungu ukifanya kazi na mimi nikitafuta kazi. Nashukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu akisema atatenda, atatenda. Kuna mambo mengi sana katika Nyahururu ambayo ningeuliza wakati Waheshimiwa wanakuja hapa wajue watu ambao walituleta hapa wanatuangalia.

Mambo ya barabara ndio haya na unajua kuna mambo mengi Mungu analeta kwa sababu nilikuwa nimekaa chini nikiona Igwamiti ikiteseka kwa sababu nilikuwa nimefungwa mikono. Sikuwa na Wadi kwa sababu nilichaguliwa kusimamia wachache lakini nimefanya yangu. Hata kama sitafanya kitu kingine.

Kutoa Nyahururu kutoka 1990 kutoka Nyandarua kuja Laikipia nitakuwa najivunia. Mjumbe wangu alisema hapana kwa sababu sijachaguliwa na watu wa Igwamiti. Nilimwambia sijafungwa midomo, mikono na miguu; kwa hivyo nitaenda nitafanya na nitanena. Hayo ni mambo mengi sana na ninajua Gavana wetu aliye na uwezo ataangalia.

Kama walimu wa Shule za Chekechea wamehitimu, ni vizuri waajiriwe kudumu. Tusiweke walimu kwa mkataba. Huyo ni mtoto kama yule wangu nimezaa. Nauliza wafanyikazi hapa ambao wameajiriwa kwa mkataba na wamehitimu wakati tutakaa na Gavana tuwatetee watu wetu. Hiyo ndio sababu tumeletwa katika Bunge hili tutetee *wanjiku*. Hatungetoshea wote katika Bunge hili lakini tumetumwa kutoka kona zote za Laikipia.

Chama zetu waliona watuletee wengine ambao tutasaidiana na wao. Hao ni ndugu na dada zetu. Bwana Spika, katika Bunge la Laikipia, nimekaa na wafanyikazi kwa miaka tano nikiwa naibu ya Meya wa Manispaa ya Nyahururu. Naomba pia wao wakule kidogo. Wakati nilikuwa naibu wa Meya nilikuwa na dereva na mlinzi na ndio nilijua hao watu wawili wana umuhimu sana. Dereva asipokula na ashibe, atakuangusha na hiyo gari yako.

Unaweza toka Bunge hili uje uulizie faili yako na ofisi ya Bwana Spika iko wapi na akose kukuonyesha. Hii ni kwa sababu tunawaona kama wao si binadamu. Nauliza Waheshimiwa wakati kitu kinatokea cha hawa wafanyikazi, tuwatetee. Kuna watu ambao nilikuwa na wao katika manispaa ya Nyahururu ambao ni Bwana Kirega na Bwana Kihanda na wengine wako mlengo ule mwingine.

Hadi wa leo wanafurahia matunda ambayo niliwapatia. Wakati wa Baraza ya Kaunti kulikuwa na pesa mingi. Nikikalia kiti, Katibu ndiye anaandika majina ya kupeana ploti.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hatukupea watu wengine. Tuliwapatia na kila mtu alitoka na ploti yake. Juzi Kihanda alitoka hapa na kwenda kuuza yake. Tuwaangalie hawa watu wakati wanafanya kazi. Ikifika ni kuwapatia gredi, watu wengine wasiwakate.

Ni vizuri wafanyikazi wapatiwe nafasi. Wengine wako hapa kwa gredi moja kama watu wa kufagia. Waongezee hata kama ni gredi moja. Tafadhali kuwa na utu ndani yako. Hata kama hakusoma na ameajiriwa hapa kama mlinzi, dereva ama mtu wa kufagia, Mungu atakubariki ukimuongezea mshahara. Wakati tunaenda michezo wachukuliwe ili wakafurahie matunda.

Bwana Spika, najua kukaa na wafanyikazi, ni wazuri kama unawachukulia kama binadamu. Hapa kutakuwa na shida kila wakati kama mfanyikazi akionekana yuko na shida anagongwa. Wako na baridi sana, kwa sababu tuko na Spika mgeni tungetaka wakati wafanyikazi wako na jambo, unawaita uongee na wao kwa sababu wako na shida zao. Wengine hawawezi kukanyaga ofisi zingine.

Mimi naongea kinagaubaga na siogopi. Naingia hapa na kusikia shida ambayo iko. Bwana Spika, waite usikize shida zao. Wengine hawawezi kukaribia kwa sababu wataandikiwa barua. Bwana Spika, jali maslahi ya wafanyikazi. Wakati tunaenda michezo usiwache watu wengine hapa ilhali hatuendi kufurahia. Kama hakuna mtu wa kufagia, kupika chai na dereva utajiendesha na gari?

Mambo mengine inafaa kuangaliwa. Bwana Spika, Mungu alikuleta hapa kama Musa ili uwaokoe wafanyikazi ilhali hawa ni watu wazuri sana. Sitaongea mengi ila naomba tufanye kazi kwa pamoja. Katika Laikipia hakuna ukabila. Hakuna chama tunaangalia kwa sababu tuliacha chama wakati tulimaliza siasa.

Bwana Spika, tukiwa na jambo na tukuite, hebu uje tuongee. Nawe ukiwa na jambo utuite tuongee tujue ni wapi tumeenda kombo ama wewe umeenda kombo. Tukiona hujaenda vizuri tukuite ukubali tuje tuketi chini. Kila boma ina shida, haiendi tu sambamba, wakati mwingine inaenda kombo. Wakati kuna shida watu wakija pamoja kazi itafanyika. Namshukuru Gavana Joshua Irungu ambaye amerudi kwa mara ya pili. Alikuwa Gavana wa kwanza na sasa tena ni Gavana wa serikali ya tatu. Tutamuunga mkono na kufanya kazi na yeye.

Jambo lingine kabla sijaketi chini ni kuhusu mambo ya kukodisha magari. Hii imeleta shida. Ukienda kule Jua Kali, kuna barabara Gavana alikuwa anatengeneza na ilikuwa tu ya siasa. Mashimo yako huko hata mtu ukiangukia ndani anajaa maji. Alisema watawekewa lami bali kilikuwa tu kitu anafanya ili apate kura. Magari mengine yako Nyahururu na mengine yako hapa kwa Gavana. Ningeomba tu haya mambo yamalizike. Kama ni ukodishaji ijulikane jinsi inavyoendelea kwa sababu ilikuwa ya watu wachache.

Nataka kuwashukuru Waheshimiwa Kibue, Veronica hata kama alitoka, Mama Yao na Jacob Endom. Sisi watano ndio tulikataa huo mkopo usipitishwe hapa kwenye hili Bunge. Tulijua kwamba huu mkopo ulikuwa wa uongo na haukuwa wa kusaidia watu wa Laikipia. Nikikuambia ukweli wa mambo mengine, wewe huwezi ukayajua. Bwana Spika, mimi ni gwiji unionavyo hapa, najua kila kitu.

Tayari walikuwa wamekula pesa wakifikiri mkopo utapitishwa. Sisi tuliukata mbele na kukosa hata kusaidiwa. Watu wengine wakasaidika nasi tukasema hata pesa yao hatuitaki. Sisi tukiwa watano hatukutaka kuonekana hapa. Wakaajiri askari wakisema tumekataa mkopo, bali

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mimi niliukataa kinagaubaga nikisimama papa hapa tu kwa sababu nilikuwa najua itakuja kuwaumiza watu wa Laikipia.

Nashukuru Mwenyezi Mungu na nakuomba, Bwana Spika, utufanyie kazi. Sisi hatuna vita na mtu bali vita yangu itatokea wakati nitaona wafanyakazi wa hapa hawashughulikiwi ipasavyo. Bwana Spika, nikiona kuna kasoro, kubali nije ofisini mwako. Mimi husimama na wafanyakazi tangu nikiwa kwenye Manispaa ya Nyahururu. Wengi hawawezi kukukaribia kukuambia shida zao. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenitoa kutoa kwa shindano la wanaume kumi na saba dhidi ya mwanamke mmoja.

Mungu alitenda na hakika kuna Mungu Mbinguni. Nataka kushukuru Mungu wangu pamoja na wale watu waliosimama nami, wahubiri wote wa Nyahururu. Mchungaji, Askofu Harrison Ng'ang'a; mimi ni Mkatoliki lakini maaskofu na makanisa yote wanajua mimi huenda kila pembe. Namwona Mheshimiwa Kanyutu anaendelea kucheka kwa sababu anajua huwa ananiita hata kwake. Asanteni, Mungu awabariki na muwe na siku njema.

Speaker: Thank you for that wonderful speech, Hon. Irene Wachuka. Indeed you have a giant ward and we respect you for that. You did a tremendous campaign and you won. We thank you, we thank God as well as the people of Igwamiti for bringing such an extremely experienced Hon. Member to the House. Thank you very much. I know that we have had good deliberations and we still have more time for that but for the time being, I will allow the Members who have not contributed time in the afternoon session to do the same.

ADJOURNMENT

Speaker: The Sittings of this House now stand adjourned until later today, Wednesday 19th October, 2022 at 2.30 p.m.

The House rose at 10.19 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*